JINA: .....NAMBARI: ..... KIDATO: .....
KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA
MAAKIZO

MAJIBU YA UFAHAMU

1. Maisha ya Evelyn na Rita yalikuwaje kabla ya Evelyn kupata kazi? (al. 2)
i. **Walikua marafiki wa chanda na pete**
ii. Walishirikiana kwa kila njia

2. Kutokana na jinsi Rita alivyomtunza Evelyn, unafikiri yeye alikuwa ni mtu wa aina gani? (al. 2)
i. **Alikuwa mwenye ukarimu**
ii. Alijawa na wema
iii. Alikuwa na mapenzi ya dhati

3. Elezabaadhiya mambo ambayo Rita alimtendeamwenzake. (al. 2)
i. **Alimnunulia mahitaji kama nguo na viatu**
ii. Alilipa kodi kwa nia baya Evelyn
iii. Alimlipia faini alipokua kizuizini

4. Baada ya kupata kazi Evelyn alikuwa mtu mkarimu. Je, unakubali?Eleza ilivyokuwa. (al. 2)
La. Evelyn alifuatilia raha za jijini na kukosa kumsaidia Rita katika kazi na gharama za maisha
5. Evelyn alipokuwamwanafunzihakuwanatabiayaudokozi. Unafikiri ni kwanini alianza tabia hiyo baada ya kuajiriwa? (al. 2)
Aliona kuwa alikuwa na pesa zake na angeweza kujikimu mwenyewe
Alidhani kuwa tayari alikuwa mtu mzima na hivyo hakuhitaji kuelekezwa
6. 'Asiyefunza na mama hufunzwa na ulimwengu.' Methali hii inahusianaje na Evelyn? (al. 1)
Evelyn alikataa kumskiza Rita na baadaye akatenda kosa lililomtia korokoroni
7. 'Akufaayekiwadhikindiyerafiki.' Methalihiiinahusianajena Rita? (al. 1)
Rita alimsadia rafikiye Evelyn alipokuwa mwanafunzi na hata baadaye alipokuwa korokoroni
8. Eleza maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumika kwenye kifungu: (al. 3)
(a) marafiki wa chanda na pete
Marafiki wasioachana kwa vyovyote vile
(b) enda mrama
Kuharibika
(c) jitolea sabili
Kuamua kikamilifu

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au sighuna. (al 2)
   (i) /t/ - **Sighuna**

   (ii) /g/ - **Ghuna**

2. Kamilisha methali zifuatazo; (al 2)

Ecolebooks.com

(i) Mgaagaa na upwa – **Hali wali mkavu**
(ii) Mvumilivu - **Hula mbivu**

3. Andika visawe vya ; (al 2)
(i) Janibu – **Kipokeo, Mkarara, Kiitikio**

(ii) Jadi – **Kale / zamani**

4. Tunga sentensi zenye maneno yafuatayo; (al 3)
(i) N + V + T
- **Watoto wawili wanatembea**

(ii) N + V + T + E
- **Mwalimu mrefu anaandika vizuri**

(iii) I + N + T
- **Lo! Juma amekuja**

5. Onyesha viambishi awali na tamati katika sentensi hizi; (al 2)
(i) Alimkaribisha

- **Awali – A – me – m** **Tamati – I - a**

(ii) Umeogelea

- **Awali – Tu – li** **Tamati - a**

6. Onyesha matumizi manne ya koma. (al 4)
(i) Kuonyesha mambo yaliyo katika orodha
(ii) Kuandika tarehe Mei 2, 2008
(iii) Kuonyesha pumziko fupi katika sentensi iliyo ndefu
(iv) Kuandika anwani
(v) Kutenga tarakimu za kiasi kikubwa 1,000,000
(vi) Kuonyesha maneno halisi yanayofuata
(vii) Katika nukuu. Akasema, " Yule kondoo ni wangu"

7. Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? (al 3)
(i) Mchungwa – **U - I**
(ii) Mdudu – **A - WA**
(iii) Bonde – **Li - YA**

8. Andika sentensi zifuatazo katika umoja. (al 3)
(i) Nyavu zimechanikachanika
- **Wavu umechanikachanika**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(ii) Nyuzi ziliingia matata
- **Uzi umaingia utata**

(iii) Fito zilikatwakatwa
- **Ufito ullikatwakatwa**

9. Andika wingi wa; (al 3)
   (i) Kiganja - **Viganja**
   (ii) Cheo - **Vyeo**
   (iii) Kibindo - **Vibindo**

10. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika wakati ujao. (al 2)
   (i) Mimi ninapenda mtoto mtiifu.
- **Mimi nitapenda mtoto mtiifu**

   (ii) Ninyi mnapendwa na wenzenu.
- **Ninyi mtapendwa na wenzenu**

11. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika hali timilifu. (al 2)
   (i) Safari hii itakuwa ndefu
- **Safari hii imekuwa ndefu**

   (ii) Shamba letu linalimwa
- **Shamba letu limelimwa**

12. Tunga sentensi ukitumia vitenzi hivi katika hali ya kutendewa. (al 2)
   (i) Kata – **Mti ulikatwa jana**
   (ii) Pasua – **Alipasuliwa mbao**

13. Eleza maana ya kirai. (al 1)
- **Ni fungu la maneno ambalo halijakamilika kimaana**

14. Onyesha kundi Nomino na kikundi tenzi katika sentensi hii. (al 2)

   Hatibu hupaswa kuifahamu lugha
- **KN – Hatibu**
- **KT – Hupaswa kuifahamu lugha**

15. Tegua vitendawili vifuatavyo. (al 2)
   (i) Kisima kidogo kimejaa changararwe
- **Kinywa na meno**

   (ii) Namsikia lakini simwoni
- **Upepo**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ISIMU JAMII (Al 10)

(i) Eleza maana ya sajili ya shuleni. (al 2)

Haya ni matumizi ya lugha katika muktadha wa shuleni.

(ii) Taja sifa nane za sajili ya shuleni. (al 8)

(i)**Sentensi ndefu – (atoe mifano katika hoja zote.)**

(ii) Huwa na mwanzilishi mkuu.

(iii)Misamiati ya taaluma mbalimbali.

(iv)kurejelea mawazo ya wengine.

(v) Lugha ya heshima/adabu.

(vi)Kuna urasmi wa lugha

(viii) Lugha iliyo na mbinu au taratibu maalum

FASIHI SIMULIZI AL 10

1. (a) Fafanua maana ya ; (al 2)

(i) Fasihi andishi

Fasihi inayowasilishwa kwa njia ya maandishi.

(ii) Fasihi simulizi

⇒ **Fasihi inayowasilishwa kwa njia ya mdomo.**

(b) Onyesha tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi. (al 8)

- ***Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo ilhali fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.***
- ***Fasihi simulizi huhifadhiwa akilini ilhali fasihi aandishi huhifadhiwa kwa maandishi.***
- ***Fasihi simulizi ni mali ya jamii ilhali fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi/mwandishi.***
- ***Fasihi simulizi ina wahusika wa kila aina k.v binadamu, wanyama na ndege, mazimwi na majitu, miungu, mizimu, mashetani na vitu visivyo na uhai k.v. mawe na miti ilhali fasihi andishi ina wahusika binadamu kwa kiasi kikubwa.***
- ***Fasihi simulizi ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi.***
- ***Uwasilishaji wa fasihi simulizi huweza kuandamana na utendaji k.v matumizi ya ishara, nyimbo, makofi, kuimba, kubeba zana katika majigambo n.k ilhali ule wa fasihi andishi hauandamani na utendaji isipokuwa inapowasilishwa mbele ya hadhira.***

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- ***Fasihi simulizi huwasilishwa mbele ya hadhira ilhali fasihi andishi si lazima iwasilishwe mbele ya hadhira.***
- ***Fasihi simulizi huwasilishwa mahali maalum k.v jandoni, matangani, arusini, n.k ilhali fasihi andishi haina mahali maalum.***
- ***Fasihi simulizi huandamana na shughuli fulani ya kitamaduni ilhali fasihi andishi haiandamani na shughuli ya kitamaduni.***
- ***Fasihi andishi huhitaji muda kutunga ilhali baadhi ya fasihi simulizi huzuka papo hapo k.m. semi, maigambo.***
- ***Fasihi simulizi ina uwezo mkubwa wa kubadilishwa na fanani anapowasilisha ufaraguzi) bali fasihi andishi haibadiliki isipokuwa mwandishi aiandike upya.***
- ***Fasihi simulizi ina historia ndefu kuliko fasihi andishi kwa kuwepo tangu mwanzo wa maisha ya binadamu***
- ***Fasihi simulizi huwasilishwa wakati maalum k.v. usiku, kipindi fulani cha mwaka ilhali andishi haina wakati maalum.***

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**